Maeneo yanayofadhiliwa na Foundation for Civil Society

Foundation for Civil Society itatoa ruzuku kwa ajili ya miradi mbalimbali ambayo inaimarisha ubora wa maisha ya maskini na walio katika mazingira magumu yanayoangukia katika katika moja ya maeneo yafuatayo,

1. USHIRIKISHWAJI/USHIRIKI KATIKA UTUNGAJI NA UTEKELEZAJI WA SERA (SERA)

Sera inaweza kufasiliwa kama misingi ya kiujumla ambayo huiongoza serikali, chama cha kisiasa, kampuni ya biashara au vyama/jumuia za kijamii katika uendeshaji wa shughuli za kitaifa au baraza la kutunga sheria kwenye maamuzi yake. Kwa maneno mengine, ni mpango au mkakati wa utekelezaji, tamko la malengo, maazimio na msimamo.

Wajibu wa jumuia za kiraia ni msingi muhimu katika kuwezesha sauti za watu kusikilizwa kwenye mchakato wa sera. Matokeo yanayotegemewa ni kuongeza uwezo wa Watanzania kushiriki kikamilifu kwenye kujadili sera na kufuatilia mchakato wa utekelezaji sera ili kuchangia kwenye juhudi za Serikali za kupunguza umaskini.

Foundation itafadhili miradi ambayo inawezesha jumuia za kiraia kushiriki katika:-

i. Michakato ya uundwaji na ufuatiliaji wa sera kwenye ngazi mbalimbali.
ii. Kushirikisha jamii katika majadiliano ya kutafuta ufumbuzi unaohusiana na sera za serikali ili kuwezesha hatua za makusudi za kutatua matatizo katika maeneo mahususi ya kijamii na kiuchumi kuchukuliwa.
iii. Usambazaji na ubadilishanaji wa habari kuhusu sera na sheria zilizopo ili kuongeza ufahamu wa jamii kuhusu sera na sheria hizo ili jumuia ziweze kuzitekeleza kwa ufanisi.
iv. Uchambuzi na ufafanuzi wa makala za sera na sheria, kwa makusudi ya kuzitafsiri ili ziweze kutumika na wananchi wa kawaida na kuzieneza.
v. Ulinganishaji wa sera na sheria mbalimbali ili kutambua vipengele ambavyo vinapingana au kuhitilafiana (ukinzani).
vi. Utekelezaji wa vipengele ndani ya sera na sheria.
vii. Ufuatiliaji wa mwenendo wa utekelezaji wa sera, sheria na programu za serikali.
viii. Kufanya tafiti zenye lengo la kuelewa kwa undani vyanzo vya misingi ya umasikini na kutoa mapendekezo yenye dhamira ya kutatua matatizo yaliyobaishwa.

ix. Kuainisha na kujadili mchango wa sekta binafsi katika upunguzaji wa umaskini.
x. Kuhimiza wananchi kupata taarifa kuhusu fursa mpya za biashara na maendeleo kama zile zinazotokana utandawazi na katika ushirikiano wa kiuchumi na mataifa jirani.

Mifano ya shughuli zilizo chini ya eneo la sera ni pamoja na:

i. Ufuatiliaji shirikishi wa utekelezaji wa mikakati na programu za kuondoa umaskini k.m. kutoa taarifa kwenye Michakato ya Mpango wa Taifa wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA).
ii. Usambazaji wa matokeo ya tafiti zilizofanyika kuhusu umasikini yakiwemo makundi yenye mahitaji maalumu, waliobaguliwa na walioachwa pembezoni.
iii. Uhamasishaji wa jamii ili kuhakiki athari za sera zilizopo au athari za mipango mahususi ya kurekebisha sera au athari za mabadiliko mengine yanayoweza kuathiri hali ya maisha ya wananchi kiuchumi na kijamii, kama katika sera za ardhi, maji, maliasili, uchimbaji wa madini, kilimo, elimu, afya, viwanda na biashara, sekta ya usafiri, sheria na usalama na kadhalika.
iv. Kuwezesha jamuia mbalimbali kushiriki kwenye kuweka vipaumbele kwa ajili ya kuboresha sera katika ngazi zote kwa mfano mikutano ya wananchi katika ngazi za chini kwa ajili ya kujadili mapendekezo mbalimbali ya sera na kupeleka wawakilishi kwa mfano mikutano inayotoa maamuzi kama mabaraza ya madiwani na bunge
v. Kuchambua sera na kuzieneza kupitia vyombo vya habari, machapisho na mikutano ya hadhara.
vi. Kutafsiri nyaraka za sera, sheria za bunge na sheria ndogo ndogo au kanuni katika lugha rahisi inayoeleweka kwa matumizi ya raia wa kawaida.
vii. Kuchunguza sera zinazopingana, kuainisha ukinzani na mapungufu na kisha kupendekeza ufumbuzi kwa mfano michakato ya kupata leseni mbalimbali, upatikanaji wa masoko ya mazao mbalimbali.
viii. Kufuatilia utekelezaji wa programu za serikali na uwekaji wa vipaumbele katika mipango ya maendeleo kwa mfano programmu ya kuendeleza elimu ya msingi (MMEM) na programu ya kuendeleza kilimo zikiwemo ahadi mbalimbali za maazimio ya kimataifa na kikanda
ix. Kuongeza ufahamu wa umma kuhusu sera na utendaji bora unaohusiana na sekta binafsi.

2. UIMARISHAJI UTAWALA BORA NA HAKI ZA KIRAIA (UTAWALA)

Utawala unaweza kufasiliwa kuwa ni utawala bora endapo unazingatia yafuatayo:

- Kuheshimu haki za binadamu
- Uwajibikaji kwa wananchi
- Utawala wa sheria
- Ushirikishwaji kikamilifu wa wananchi na makundi yote
- Uwazi na ukweli
- Michakato na taasisi zinazowajibika ndani na nje
- Sekta binafsi na za umma pamoja na asasi za jamii zenye ufanisi na zenye kuleta matokeo yanayotegemewa
- Upatikanaji wa maarifa, taarifa na elimu kwa watu wote
- Uwezeshaji watu kisiasa, haki, uendelevu na mitazamo na maadili ambayo yanaendeleza uwajibikaji, mshikamano na kustahimiliana.

Jumuia za kiraia ni muhimu katika kuhakikisha kwamba taasisi za umma na za binafsi zinafuata misingi iliyotajwa hapo juu na kusaidia watu kufahamu haki na wajibu wao. Matokeo yanayotegemewa ni kuwepo kwa Serikali, taasisi za umma na za binafsi zenye mipango endelevu, zinazofanya kazi kwa uwazi, ufanisi, zinazowajibika kwa watu zinazowatumikia, na zinazoheshimu utawala wa sheria na haki za binadamu pamoja na jamii ambayo inafahamu haki na wajibu wake.

Foundation itafadhili shughuli ambazo:

i. Zinakuza uelewa wa haki za binadamu na uwajibikaji wa serikali,
ii. Zinakuza uelewa wa wajibu na majukumu ya kiraia, taasisi za sekta binafsi na Asasi Zisizo za Kiserikali na za kijamii zinazojitegemea.
iii. Zinajumuisha haki za binadamu kwenye programu yoyote ya maendeleo, sera, sheria au mradi.
iv. Zinajumuisha upenyezwaji masuala ya jinsia (mwelekeo tawala) kwenye programu yoyote ya maendeleo, sera, sheria au mradi.
v. Zinahimiza tafiti na pia kusambaza matokeo ya tafiti zinazohusu aina mbalimbali za utawala kwenye taasisi za umma na za binafsi kwa lengo la kutatua matatizo muhimu yanayohusika.
vi. Zinaongeza upatikanaji wa haki kutoka mamlaka za sheria hususani kwa watu maskini.
vii. Zinakuza ufahamu kuhusu kazi za ushirikishwaji wa jamii na wajibu wa kiraia.
viii. Zinaendeleza programu za elimu ya demokrasia, uchaguzi na elimu ya wapiga kura.
ix. Zinaboresha mifumo ya kuwa tayari ili kuweza kudhibiti majanga kwenye ngazi mbalimbali za kitaasisi.
x. Zinaboresha udhibiti wa migogoro kwenye ngazi mbalimbali za jamii.

xi. Zinaboresha na kuwezesha upatikanaji na upashanaji wa habari na taarifa kati ya taasisi mbalimbali.
xii. Zinaendeleza haki za watu kujiunga na kufanya kazi pamoja.
xiii. Zinaboresha uelewa wa mienendo ya kimataifa, kikanda na kitaifa hususani kwenye masuala ya biashara, viwanda, upatikanaji masoko ya bidhaa na biashara ndogo ndogo.

Mifano ya shughuli zilizo chini ya eneo la Utawala Bora ni pamoja na:-

i. Programu kwenye vyombo vya habari kuhusu masuala ya utawala bora kama vile rushwa, uwajibikaji, uwazi, utawala wa sheria, ufanisi, demokrasia na haki za binadamu.
ii. Sanaa shirikishi kuhusu haki na wajibu wa taasisi za umma na za binafsi kuanzia ngazi ya familia mpaka taifa.
iii. Midahalo juu ya haki na wajibu wa raia kwa mujibu wa Katiba ya nchi.
iv. Programu za kuchunguza matatizo ya utawala bora na kubuni ufumbuzi unaowezekana kutatua matatizo hayo kama rushwa, unyanyasaji wa kijinsia, upendeleo wa kikabila katika sehemu za kazi nk.
v. Mafunzo kwa jumuia za kiraia, viongozi wa serikali kuu na za mitaa kuhusu programu mbalimbali za marekebisho ya sera, sheria na uchumi, kama vile, marekebisho ya sekta ya umma, marekebisho ya serikali za mitaa, na marekebisho ya sekta ya sheria.
vi. Kuwasilisha mahakamani mashauri maalumu kuhusu haki ya umma na yenye kugusa wananchi walio wengi kuhusiana na masuala muhimu ya utawala bora na haki za binadamu.
vii. Utengenezaji wa machapisho yenye Elimu na Mawasiliano juu ya masuala ya utawala bora na haki za binadamu.
viii. Uwezeshaji wa utoaji huduma za kisheria kwa masikini kama vituo vya Msaada wa Kisheria na huduma zenye mwelekeo wa kisheria.
ix. Kujenga uwezo wa jumuia za kiraia kuendesha mambo yao wenyewe na kuwa mfano mzuri wa utawala bora.
x. Kuongeza ufahamu kuhusu vyombo vya dola na haki za binadamu.
xi. Mafunzo kwa wafanyakazi wa taasisi mbali mbali na jamii kwa ujumla kuhusu uthibiti wa majanga kama vile mafuriko, njaa, n.k. na namna ya kujiweka tayari kukabiliana na majanga hayo.
xii. Upatikanaji wa taarifa muhimu na kuzibandika kwenye mbao za matangazo katika vijiji au vitongoji mijini k.m. kuhusu afya, elimu, taarifa za akaunti za serikali za mitaa, bei za mazao na matukio muhimu.
xiii. Uanzishaji wa hifadhi wa taarifa na takwimu kuhusu ukiukwaji wa haki za binadamu, usambazaji wa taarifa hizo na uboreshaji wa uwezo wa jamii kuwa wasimamizi wa mambo yanayowahusu.

xiv. Kuongeza fursa za ushirikishwaji kikamilifu wa Watanzania kwenye uendeshaji wa sekta binafsi.

3 UKUZAJI WIGO WA USALAMA NA MSAADA KWA WANAOWEZA KUATHIRIKA ZAIDI NA UMASIKINI
(MITANDAO YA USALAMA)

Wigo wa Usalama unaweza kufasiliwa kama utoaji msaada kwa wanajamii ambao wameachwa pembezoni kwenye shughuli za kimaendeleo, na kwa hiyo wana uwezekano mdogo wa kufaidika na rasilimali za jamii inayowazunguka. Kwa maneno mengine, watu kama hao hawawezi kufaidika kutokana na mikakati ya kiujumla ya upunguzaji umaskini na ukuzaji uchumi. Kwa kuwa kuna uwezekano wa mtu, kaya au jumuia kuathirika kutokana na kudumaa kwa ustawi wa hali zao. Inahitajika mipango ya muda mrefu inayolenga kushughulikia vyanzo vya msingi vya uwezekano wa jamii kudhurika zaidi kutokana na hali ya maisha yao kudumaa. Shughuli za muda mfupi ni zile zinazolenga utoaji wa huduma za moja kwa moja kwa waathirika.

Asasi na jumuia za kiraia zinatoa mchango mkubwa katika kuwapatia kinga kundi ambalo linaweza kudhurika zaidi. Kuna umuhimu wa kuweka utaratibu ambao wanaweza kuutumia ili kueleza masuala yao na kuboresha hali zao za maisha. Taasisi za kijamii pia hutoa mchango mkubwa kwenye kulinda wanaoweza kudhurika zaidi kutokana na athari za umaskini. Mitandao ya kijamii inaweza kuongezwa nguvu ili kuwawezesha masikini kufanya kazi pamoja ili waweze kutimiza malengo yao ya pamoja. Matokeo yanayotegemewa ni jamii ambayo iko katika hali ambayo ushiriki wa watu ambao wako katika hatari ya kudhurika na umasikini inaongezeka katika michakato ya maendeleo kwenye ngazi zote.

Foundation itafadhili programu ambazo zitapanua upeo wa wanaoweza kudhuriwa na umasikini au majanga mengine kwa kuwaleta pamoja na kuwashirikisha kwenye programu za maendeleo kupitia:

i. Kuimarisha uwezo wa asasi, jumuia za kiraia ambazo wanachama wake ni pamoja na wale wanaoweza kuathirika zaidi na umaskini.
ii. Programu ambazo zinatambua na kushughulikia viwango vya uwezekano wa kudhuriwa kwa lengo la kuvipunguza na uendelezaji wa uwajibikaji wa jamii.

iii. Kushughulikia vitendo ambavyo vinawaongezea nguvu wanaoweza kudhuriwa vyenye lengo la kugeuza mwelekeo na kuweka mikakati ya ushirikishi.
iv. Shughuli ambazo zinasaidia wanaoweza kudhuriwa kutafuta ufumbuzi wa kudumu wa matatizo yao.
v. Kusaidia kujenga mitandao ya wanaoweza kudhuriwa ndani ya jumuia za wenyeji wa mahali fulani na mitandao ya misaada ya kijamii kati ya jumuia k.m. akina mama wanaolea watoto peke yao, watu wanaoweza kuathirika na wanaoishi na virusi vya ukimwi, yatima, wajane, watu wenye ulemavu, akina mama waja wazito, waliopata maafa na wazee.
vi. Kulenga wale walio katika hatari ya kuathirika na umasikini pamoja na kuachwa nyuma kwa wazee katika shughuli za maendeleo na huduma.
vii. Kuimarisha uwezo wa jumuia za kiraia katika kuhudukia makundi yaliyo katika hatari zaidi.

Mifano ya shughuli zilizo chini ya mada ya wigo wa Usalama ni pamoja na:

i. Kuwezesha uanzishwaji wa mitandao ambayo wale wanaoweza kudhuriwa ni wanachama washiriki na ndio wanaonufaika.
ii. Kuboresha uelewa wa jumuia za kiraia kuhusu dhana nzima ya makundi yenye uwezekano wa kudhurika, kutoshirikishwa na kuwekwa pembeni katika shughuli za maendeleo na pia kuboresha uwezo wa kubuni mikakati inayofaa ya kupunguza umaskini katika jamii.
iii. Kukuza uelewa, kutoa msaada na kuwatunza waadhirika wa VVU/UKIMWI, malaria na matumizi mabaya ya madawa ya kulevya, ukatili dhidi ya watoto, unyanyasaji na ukatili wa kijinsia, mimba za utotoni, mila na desturi zenye madhara.
iv. Programu za kujitayarisha kukabili mapema majanga endapo yanatokea.

v. Programu za vijana ambazo zinapunguza uwezekano wa kuathirika kwa mfano michezo, kujifunza kwa kutumia mifano hai, urejeshwaji wa uadilifu, ujenzi wa kujiheshimu na kujiamini, usimamiaji mzuri wa msongo wa mambo na matumizi mazuri ya muda, uzuiaji wa uhalifu, msaada kwa wafungwa waliomaliza vifungo, afya ya uzazi na stadi za uongozi.
vi. Programu za kufanya kazi na jamii kutambua njia za ukulima zinazofaa kwa mfano mbadala wa mbolea za viwandani.
vii. Programu za kuangalia madhara ya mimba kwa vijana wadogo wa kike, ukeketaji nk.
viii. Upelekaji taarifa muhimu kwa walengwa wanaozihitaji kwa mfano breli kwa vipofu, lugha ya ishara kwa viziwi na uwezeshaji wa walemavu wengine.
ix. Ujenzi wa uwezo unaohusu mienendo bora katika kuwahudumia wanajamii wanaoweza kudhuriwa.

x. Kushughulikia unyanyapaa kwa watu wanaoishi na virusi vya ukimwi na kuzuia ubaguzi wowote.

4 KUIMARISHA UWEZO WA USHAWISHI, UTETEZI NA UANZISHAJI NA UENDELEZAJI MITANDAO YA JUMUIA ZA KIRAIA.

(UIMARISHAJI WA UTETEZI)

Lengo la ushawishi na utetezi ni kuleta na kuendeleza mabadiliko ya kweli ya kijamii na kiuchumi ili kufikia lengo fulani lililowekwa. Lengo la eneo hili ni kuifanya jamii ya kiraia ionekane na ishiriki kikamilifu katika kuleta mabadiliko muhimu kwenye jamii.

Kuboresha uwezo wa ushawishi wa mitandao wa vyama vya hiari vya kijamii ili kuleta matokeo yanayotarajiwa. Wakati huo huo, taasisi moja moja zinahitajika kuboresha uwezo wa kushawishi kikamilifu na kupata mafanikio. Matokeo yanayotegemewa ni jamii ya kiraia yenye usanifu, ubunifu na iliyo hai na ambayo inatoa mchango kikamilifu kwenye kuleta mabadiliko ya kudumu kwenye maendeleo ya Tanzania.

Foundation itafadhili shughuli ambazo:

i. Zinasaidia jumuia za kiraia kutafuta nafasi yao kwenye michakato ya maendeleo na upunguzaji wa umasikini.
ii. Zinasaidia jumuia za kiraia kutangaza kazi zao na michango yao katika michakato ya maendeleo.
iii. Zinaongeza nguvu ubia, muungano na mitandao ili kushirikiana kushughulikia masuala mahususi na misukumo na mada zinazohusiana na hayo katika ngazi ya kitaifa na kimataifa.
iv. Zinakuza stadi na uelewa kuhusu ushawishi na utetezi wa sera, utawala bora, demokrasia na haki za binadamu.
v. Zinajenga uwezo wa jumuia za kiraia kuhusu uandaaji miradi, utekelezaji, ufuatiliaji na ufanyaji tathmini ya miradi hiyo.
vi. Misaada ya kitaalamu kwa ajili ya jumuia za kiraia kujizatiti na kukuza uwezo wa watendaji wake.
vii. Kusaidia umma kushiriki kikamilifu kwenye kutathmini utendaji kazi na programu za jumuia za kiraia.

Mifano ya shughuli zilizo chini ya eneo la Uimarishaji ni pamoja na:-

i. Programu za kutembeleana na kubadilishana mawazo na uzoefu kati ya taasisi za ushawishi.
ii. Mafunzo ya kuboresha stadi ambazo zitaongezea nguvu mitandao k.m. mabadiliko kwenye vikundi na utawala, ushirikiano wa kitaasisi, mikakati ya ushawishi na utetezi, na mitindo ya menejimenti ya kisasa inayoshughulikia zaidi matokeo.

iii. Mafunzo juu ya uchanganuzi wa sera, dhana za demokrasia, haki za binadamu, utawala bora, na makundi yenye uwezekano wa kudhuriwa, kuwekwa pembezoni na ushawishi na utetezi.
iv. Uundaji wa mfumo na usambazaji wa Taarifa, Elimu na Mawasiliano (TEM) ambao unalenga wananchi maskini.
v. Uanzishaji wa vituo vya kutolea na kupata taarifa kwa ajili ya wananchi.
vi. Utoaji taarifa kupitia vyombo vya habari, kuchapisha vijarida au kutumia mitandao ya kompyuta k.m. intaneti.
vii. Kufanya ushawishi ili kupata uwakilishi wa jumuia za kiraia kwenye vyombo vya kufanya maamuzi k.m. Bunge, Halmashauri za Wilaya, na mabaraza ya vijiji.
viii. Kuangalia upya na kutathmini ufanisi wa menejimenti za jumuia za kiraia kwa nia ya kukuza ufanisi na kupata matokeo yanayotarajiwa.
ix. Kusaidia mtandao wa wakulima au wafanyabiashara kupata taarifa muhimuzinazowahusu kwa mfano vyama vya ushirika.

Kwenye maeneo yote hapo juu, umuhimu unaelekezwa zaidi kwa watu masikini na wale wamakundi yanayoweza kuathirika zaidi na umasikini. Programu bunifu zitapewa umuhimu wa hali ya juu.